

Chanjo ya COVID-19

Chanjo ni nini?

Chanjo ni aina ya dawa. Inakuja kwenye sindano au shuti.

Chanjo hufanya nini?

Kupata chanjo hukuepushana na kuugua. Kuna aina tofauti za chanjo za maradhi au magonjwa tofauti.

Je, chanjo ni salama?

Ndiyo. Madaktari na wanasayansi hufanya kazi kwa bidii kuhakikisha chanjo ni salama. Chanjo tu ambazo ni salama ndizo zinazoidhinishwa kutumiwa nchini Kanada. Usalama wa chanjo hukaguliwa mara nyingi.

Je, kuna chanjo ya COVID-19?

Ndiyo, kuna chanjo mpya chache za COVID-19.

Je, ni chanjo gani iliyo bora zaidi?

Chanjo zote zinasaidia sana kupunguza hatari ya kuambukizwa COVID-19. Ikiwa utaambukizwa COVID-19 baada ya kuchanjwa, chanjo hiyo pia itakupunguza hatari ya wewe kuwa mgonjwa sana. Madaktari wanawahimiza watu kupokea chanjo ya kwanza inayopatikana.

Je, chanjo za COVID-19 ni salama? Zilitengenezwa haraka sana.

Ndiyo. Madaktari na wanasayansi walifanya kazi kwa bidii kuhakikisha chanjo za COVID-19 ziko salama. Chanjo tu ambazo ni salama ndizo zinazoidhinishwa kutumiwa nchini Kanada. Usalama wa chanjo hukaguliwa mara nyingi.

Je, ninaweza kuambukizwa COVID-19 kupitia chanjo?

La. Huwezi kuambukizwa COVID-19 kupitia chanjo. Chanjo husaidia mwili wako kutambua na kupambana na COVID-19.

Je, kuna athari mbaya za chanjo ya COVID-19?

Baada ya kupata chanjo, huenda ukaathirika. Mkono wako unaweza kuwa na uchungu mahali ulipodungwa

sindano. Huenda ukajihisi mchovu au mwenye joto jingi. Hii inamaanisha mwili wako unakubali chanjo. Athari hizi zinaweza kukaa kwa siku chache.

Watu wengine wanaweza kuwa na mzio wa chanjo. Watu wanaweza kuwa na athari mbaya zaidi. Athari hizi kali ni nadra.

Je, ikiwa dalili zangu zitakaa zaidi ya siku chache?

Huenda ulikuwa umeambukizwa virusi kabla ya kupata chanjo. Ikiwa dalili zako zitakaa zaidi ya siku moja au mbili, huenda umeanza kuugua. Unapaswa kujitenga (jijepushe na watu wengine) na upimwe COVID-19.

Ninaweza kupata chanjo lini?

Unaweza kuipata sasa. Kuna nafasi za kuweka miadi kote kwenye mkoa. Unaweza kupiga simu ili kuweka miadi kupitia nambari 1-844-626-8222 (1-844-MAN-VACC). Kuna wakalimani wa simu kwa lugha mia nyingi wanaoweza kukusaidia unapohifadhi nafasi na vile vile kwenye mitandao. Unaweza kupata maelezo zaidi kwenye manitoba.ca/vaccine au protectmb.ca.

Je, ni lazima niendeele kuvaa maski na kukaa mbali na watu wengine nikipata chanjo?

Ndiyo. Kuvaa maski na kutokaribiana na watu kutakusaidia kukulinda na kuwalinda wengine.

Je, ninahitaji kulipia chanjo?

Chanjo inatolewa bila malipo kwa watu wa Manitoba.

Je, ni lazima nipate chanjo?

Chaguo ni lako ikiwa ungependa kupokea chanjo ya COVID-19. Sio lazima upokee chanjo.

Watu wengi wana maoni tofauti kuhusu chanjo hiyo. Maelezo mengine huenda si ya kweli. Unaweza kuzungumza na watoa huduma za afya ili upate maelezo zaidi kuhusu chanjo. Watakupa maelezo sahihi.

Unaweza pia kutembelea manitoba.ca/vaccine ili upate maelezo.

Manitoba 